**Learning by Ear 2010 "Against the Current Urban Exodus"**

**Episode 03: "The daily bread"**

**Author: Alfred Dogbé**

**Editor: Yann Durand**

**Translator: Anne Thomas**

WAHUSIKA:

Scene 1:

- **TINGO** (UMRI MIAKA 32, MKULIMA WA KISASA, AMEJITOSHELEZA)
- **BAKI** (UMRI MIAKA 26, MWANAELIMUJAMII, RAFIKI YAO ZEINA NA BEN)
- **ZEINA** (UMRI MIAKA 24, MCHUMI, RAFIKI YAO BAKI NA BEN)

Scene 2:

- **BEN** (MHANDISI WA KILIMO, UMRI MIAKA 29)
- **KABO** (MKULIMA, MJOMBAKE BEN, UMRI MIAKA 57)

Scene 3:

- **BEN** (MHANDISI KILIMO, UMRI MIAKA 29)
- **KABO** (MKULIMA, MJOMBAKE BEN, UMRI MIAKA 57)
- **BAKI** ( UMRI MIAKA 26, MWANAELIMUJAMII, RAFIKI YA ZEINA NA BEN)
- **ZEINA** (UMRI MIAKA 24, MCHUMI, RAFIKI YAO BAKI NA BEN)

**Intro:**

Karibu kwenye mfululizo huu mpya wa vipindi vyetu vya Learning by Ear kuhusu uhamiaji mijini, uitwao “Kukabiliana na Wimbi la Mabadiliko”. Hili ni jambo geni sana. Lakini ni hatua inayoweza kuwasaidia watu kuondokana na ukosefu wa kazi katika miji mikubwa.

Tunafuatiliza masaibu ya Ben, Baki na Zeina - vijana watatu wasio na kazi walio na shahada za chuo kikuu wanaotaka kuanzisha chama cha ushirika cha ukulima kijijini..

Kwenye kipindi hiki cha tatu utashuhudia jinsi vijana hawa walivyotiliwa shaka kijijini mwao walipoamua kurudi huko kutoka mjini.

**Scene 1: In the village. Tingo's farm.**

**TINGO, BAKI AND ZEINA.**

1. **ATMO: FARM SOUNDS. NOISE OF A TRACTOR GOING AWAY**
2. **ATMO: MEN SING WHILE THEY WORK TO THE RYTHMIC SOUND OF THE SWEEPING MACHETE**
3. **TINGO** Haya basi, unalionaje shamba langu?
4. **BAKI** Zuri!
5. **ZEINA** Siamini kwamba hapa ni kijijini kwetu!

**6.** **TINGO** Mambo hayafanyiki tu jijini!

**7.** **BAKI** Nimeshangaa sana. Nilipoondoka kijijini, shamba hili halikuwa shamba la kupigiwa mfano.

**8.** **TINGO** Hili shamba lilitokana na mihemko wakati wa kupata uhuru. Lakini unajua hali ilivyo humu nchini. Kila kitu husambaratika baada ya miaka kumi hivi. Nilipolitwaa shamba hili miaka kumi iliyopita, watu walidhani nina kichaa!

**9.** **BAKI** Haya yote umeyafanya kwa muda wa miaka sita?

**10.** **TINGO** Miaka sita ya mwanzo niliajiri wafanyikazi wawili wa kudumu na sasa hivi wako 30. Wakati wa mavuno mimi huwapa watu kiasi 250 kazi za vibarua. Nina matingatinga mawili na mtambo maalumu wa kujaza magunia, kuyapima uzani na pia kuweka vibandiko.

**11.** **ZEINA** Umefanya jambo la maana!

**12.** **BAKI** Kweli hilo! Hongera!

**13.** **TINGO** Asante. Lakini nakwambia haikuwa rahisi vile!

**14.** **ZEINA** Kwa nini?

**15.** **TINGO** Mvua haitabiriki, lakini hapa tumebahatika. Mtu hachimbi ardhi kina kirefu kupata maji. Nilipata mkopo wa fedha nikakikarabati kisima na mtambo wa kunyunyizia maji shamba.

**16.** **BAKI** Lakini nasikia mabenki hayafadhili uwekezaji kwenye kilimo.

| | | |
|---|---|---|
| **17.** | **TINGO** | Hilo si kweli. Inakubidi uwahakikishie mradi wako unafaa na utaleta manufaa. |
| **18.** | **BAKI** | Unakuza njugu-karanga tu? |
| **19.** | **TINGO** | Ndio. Zina kazi nyingi lakini pia zina faida. Hata hivyo, sasa hivi bei yake inazidi kushuka. Lakini nashukuru Mungu sijatatizika. Mwaka uliopita niliuza njugu zenye ujazo wa zaidi ya milioni 60. |
| **20.** | **BAKI** | Mavuno yako ya njugu unayauza wapi? |
| **21.** | **TINGO** | Ulaya. Mwanzoni mwa msimu huwa tunashauriana kuhusu kiasi kinachohitajika kisha tunapeleka bidhaa baada ya mavuno. Huwa wanaingiza hundi kwenye akaunti yangu. Siwajui wateja wangu lakini ni washirika wa kuaminika. |
| **22.** | **ZEINA** | Shamba lako lina uwezo wa kulisha watu wote kijiji kizima. |
| **23.** | **TINGO** | Hata zaidi! |
| **24.** | **BAKI** | Mbona hujishughulishi na mazao ya vyakula, matunda, mboga na nafaka? |
| **25.** | **TINGO** | Wanaonunua na kulipa hawali mawele na mtama. |
| **26.** | **ZEINA** | Lakini tukikosa kuwa na mpango madhubuti wa kukuza mimea ya chakula, hatutawahi kukabiliana na upungufu wa chakula humu nchini. |
| **27.** | **TINGO** | Hilo ni kweli na ni mwenendo mzuri. Lakini hali ndiyo inayotusababisha kufanya tufanyavyo. |

| | | |
|---|---|---|
| **28.** | **BAKI** | Mimi si mtaalamu, lakini inaonekana udongo wa shamba lako umeendelea kukosa rutuba. Huoni kwamba hilo latokana na kutumiwa zaidi pamoja na ukuzaji wa aina moja tu ya mmea wa mazao? |
| **29.** | **TINGO** | Ni tatizo kubwa lakini huwezi kula yai bila kulivunja… |
| **30.** | **ZEINA** | Ukiendelea hivi, miaka kumi ijayo hutaweza kukuza kitu chochote kwenye shamba lako hili! |
| **31.** | **TINGO** | La muhimu ni kupata fedha nyingi SASA. Kwa hivyo itakuwa rahisi kununua shamba jingine. Na hali ya umasikini tuliyo nayo huwezi kukosa watu wanaotaka kuuza mashamba yao. |
| **32.** | **ZEINA** | Ukizingatia uwezo ulio nao, unaweza kubadilisha mambo kwa kiasi kikubwa. |
| **33.** | **TINGO** | Watu wengi hutaka kufanya kila kitu. Wanataka pia kufanya kazi za wengine. Hilo ni kosa. Mimi ni mfanyabiashara. Jukumu langu ni kujifaidi kifedha wala si kuingilia siasa. Na nyinyi ni wahitimu wa vyuo vikuu. |
| **34.** | **BAKI** | Naam, na tumeamua kurejea kijijini |
| **35.** | **TINGO** | Huo ni ujasiri wa hali ya juu! Kwa jumla, watu huchukulia kwamba watu kama ninyi wenye shahada za vyuo vikuu hawataki kuondoka mjini. Ilhali ni ukweli usiopingika kwamba hata hapa tunauhitaji ujuzi wenu! |
| **36.** | **ZEINA** | Hivyo ndivyo tunavyokisia. |

**37. TINGO** Huku kuna kazi. Tena nyingi. Nahitaji watu kama ninyi wenye ujuzi wa hali ya juu. Je, mna vyeti vyenu?

**38. BAKI** Kusema la haki, hatutaki kuajiriwa na mtu.

**39. ZEINA** Tunataka kuanzisha chama chetu cha ushirika wa kilimo.

**40. TINGO** Wapi? Hapa, kijijini?

**41. ZEINA** Ndiyo. Tunataka kuimarisha stadi zetu na kusaidia kuikuza kilimo hapa kijijini.

**42. TINGO** Nawaambia mtabadilisha hayo mawazo yenu! Nadharia ya chuo kikuu ni tofauti na hali halisi. Lakini nafasi ninazo, kama mnataka ajira yenye mshahara mkubwa. Nimefurahi kuonana nanyi lakini sasa hivi naomba nirejee kazini.

**----- MUSIC -----**

**Scene 2: In the village. Kabo's home.**

**KABO AND BEN**

**43. SFX : CHILDREN PLAYING – MOTORBIKE NOISE – CONVERSATION IN THE DISTANCE**

**44. KABO** Kila mtu hapa kijijini anatamani kukimbilia mjini. Kuondokana na dhiki. Kwenda mahali ambapo mtu hakumbani na njaa na fedheha. Na wewe, ati umeamua kurejea huku? Kwani umerogwa?

**45. BEN** Mjomba, tafadhali nisikize! Ebu tulia kidogo usikie ninayokwambia!

| | | |
|---|---|---|
| **46.** | **KABO** | Haya, zungumza ninakusikiliza! |
| **47.** | **BEN** | Mimi na marafiki zangu wawili tumeamua kurudi kijijini kuanzisha na kukisimamia chama cha ushirika cha ukulima. |
| **48.** | **KABO** | Una maana gani hasa? |
| **49.** | **BEN** | Mjomba, kazi yangu inahusisha pia kuwasaidia wakulima kuimarisha kazi zao. Tutafanikiwa kukabiliana na njaa na fedheha. Itakuwa kwa faida yetu na jamaa zetu. Ndio maana tulihudhuria shule. |
| **50.** | **KABO** | Sijali iwapo mtafanya kazi ya shamba. Lakini shamba gani? Tumepoteza karibu kila kitu. Baba yako hajakuambia? |
| **51.** | **BEN** | Kwa hakika, hilo la ardhi halijanishughulisha kwa sababu sijawahi kuwa na fikra ya kuja kuishi kwenye ardhi hiyo. |
| **52.** | **KABO** | Huo ulikuwa uamuzi mzuri! |
| **53.** | **BEN** | La, hasha! Niliipuuza asili pamoja na utambulisho wangu. Nasikitika kwamba shuleni nilijifunza kuwa naweza kujiendeleza na kuishi nikiwa kijijini kwangu. Hakuna atakayekuja kuendeleza kijiji chetu ila sisi wenyewe. |
| **54.** | **KABO** | Wewe na marafiki zako mna wazo zuri. Ni heshima kubwa kwenu. Lakini ningedhani nyinyi ni watu wa kufanya kazi kwenye afisi kubwa zilizo na viyoyozi. Huko ndiko mngeweza kulinda hadhi zenu na kutusaidia sisi. Wahenga wanasema: lazima uwe nacho ndipo utoe. |

| | | |
|---|---|---|
| **55.** | **BEN** | Hatujaja kumsaidia yeyote kifedha. Tumekuja kwa kauli moja: Njooni, tufanye kazi pamoja! Tuna nia,ujuzi pamoja na mawasiliano na vinaweza kutusaidia. Lakini tunanchokitaka hasa ni kutuunga mkono na kushiriki. |
| **56.** | **KABO** | Kwa kweli tuna mengi ya kujifunza kutoka kwenu. Utadhani ndiyo mara ya kwanza mimi na wewe tumeanza kuwasiliana. Laiti tungejua mapema! |
| **57.** | **BEN** | Ni kosa langu pia, kwani sikushauriana nawe sana. |
| **58.** | **KABO** | Si neno! Bado kuna muda.Wenzako ninaowafahamu wako wapi? |
| **59.** | **BEN** | Utawatambua. Tulikuwa pamoja kabla ya kuondoka kwenda masomoni mjini. Sasa hivi Zeina na Baki wamo shambani kwa Tingo. |
| **60.** | **KABO** | Mnafanya nini kwake? |
| **61.** | **BEN** | Kwani ana nini? |
| **62.** | **KABO** | Huyo bwana ni shetani mkubwa! Amevuruga kila mtu hapa. Alituhadaa kwamba angetukopesha fedha lakini ameishia kumiliki mashamba yote hapa kijijini. Ni jambazi. Mkishirikiana naye kijiji kizima kitawapuuza. |
| **63.** | **BEN** | Hatushirikiani naye. Hata hivyo yeye ndiye msimamizi wa shamba la pekee hapa linalotumia mbinu za kisasa. Ndiposa tukaamua tutazame shughuli zake. |
| **64.** | **KABO** | Ningependa kusikia maoni ya marafiki zako. |

**65. BEN** Basi tuandamane hadi kwenye uwanja wa kijijin - nitakutana nao huko.

**----- MUSIC -----**

**Scene 3: At the village square.**

**KABO, BEN, BAKI AND ZEINA.**

**66. ATMO: SHOUTS AND LAUGHTER FROM CHILDREN PLAYING. WANDERING SALESPEOPLE. COWS MOOING IN THE DISTANCE**

**67. BEN** Mjomba Kabo, hawa ni marafiki zangu ambao pia ni washirika wangu. Huyu ni Zeina.

**68. ZEINA** Ninafurahi kujuana nawe.

**69. BEN** Na huyu ni Baki!

**70. BAKI** Hujambo.

**71. KABO** Ben amenieleza mambo mengi kuhusu mradi wenu. Ningependa kuwahimiza muendelee vivyo hivyo na pia ninawatakia kila la heri.

**72. ZEINA & BAKI** Asante sana.

**73. BEN** Sijafanikiwa kukutana na msimamizi wa idara ya maendeleo ya mashambani.

**74. BAKI** Mbona? Kwani hakutaka kukutana nawe?

**75. BEN** Hapana. Hakuwepo. Nitarudi tena.

**76. KABO** Usimtafute ofisini mwake. Afisi yake ni kwenye baa ya hapa kijijini.

**77. BEN** Alaa! Sikujua hilo. Na nyinyi je? Mlikutana na Tingo?

**78. BAKI** Zeina, mweleze wewe maana kila nikikumbuka.... (**FIT OF HYSTERICS**)

**79. BEN** Kwani ilikuwa vipi?

**80. ZEINA** Alidhani kwamba tunamwendea kuomba kazi. Na alipofahamu tunataka kuingilia sekta anayoishughulikia na kuwashauri wanakijiji, hakutaka tuendelee na mazungumzo!

**81. BAKI** (**still laughing**) Nina hakika kwamba ndiyo mara yake ya kwanza ametembelewa na watu ambao si ombaomba. Ajabu!

**82. KABO** Kwa nini mlimtembelea?

**83. BAKI** Tulitaka kupata fununu kuhusu hali katika eneo lake. Tuone anavyoshughulika nasi tujifunze kutokana na hilo. Hivyo tu.

**84. ZEINA** Hatutashirikiana naye. Huyo bwana ni tapeli.

**85. KABO** Mnapaswa kujihadhari naye. Ni nyoka! Tayari nimeshamweleza Ben. Tingo amevuruga nusu ya kijiji chetu.

**86. BAKI** Ni dhahiri kwamba itatubidi kuanzisha chama cha ushirika ili kukabiliana naye na mbio zake za kutaka kujitajirisha kwa kuwapunja wanakijiji. Na kwa kuharibu mazingira.

**87. KABO** Kama hilo ndilo lengo lenu. Kijiji kizima kitawaunga mkono. … Ninadhani kutakuwa na mabadiliko makubwa hapa. Nitawasaidia. Nitajaribu juu chini kuwavutia watu wengi iwezekanavyo wakiunge mkono chama chenu. Inshaallah!

**Outro:**

Na huo ndio mwisho wa kipindi cha *Learning by Ear* hii leo. Tunakushukuru kwa kutegea sikio kipindi cha tatu cha "Kukabiliana na Wimbi la Mabadiliko" kwenye mfululizo wetu wa uhamiaji mijini.

Usikikose kipindi chetu kijacho ambapo utafahamishwa jinsi Ben na kundi lake walivyofanikiwa kuwajumuisha wanakijiji kwenye harakati zao za kuanzisha chama cha ushirika.

Iwapo ungetaka kukisikiliza tena kipindi hiki au kutupatia maoni yako fungua ukurasa wetu wa tovuti dw-world.de/LBE au utuandikie barua-pepe kupitia anwani: lbe@dw-world.de.

Usikose kusikiliza kipindi kijacho!

**END OF EPISODE 3**